



## **Njia Mpya Za Kujikinga**

Ukimwi si ugonjwa mpya. Ugonjwa wa ukimwi umetangazwa na manyumba za utangazaji duniani kwote kwa zaidi ya miaka thelathini na bado inaendelea. Mwaka wa elfu mbili na sita kesi mpya za virusi milioni nne na laki tisa zilitangazwa na milioni mbili na laki tisa waliaga dunia. Asilimia tisaini na tano (95%) ya watu wanao virusi vya ukimwi wanaishi Afrika na asilimia tisaini (90%) hawajui hali yao ya ugonjwa wa ukimwi. Kwa sasa ukimwi hauna dawa lakini hii ripoti inaonyesha vile madawa na kutairisha wanaume inateremsha nafasi ya kueneza virusi vya ukimwi duniani.

Kwa hivi sasa hakuna dawa ya ukimwi lakini njia nyingi zinafanyiwa utafiti. Njia za kujikinga kwa ukimwi yaani kwa kutumia madawa ili virusi ishikushike ndio njia halisi ya kujikinga kwa virusi hivi lakini bado ni ngumu kufanya kwani ni lazima ifanyiwe utafiti wa kutosha kwa muda mrefu na pia ina gharimu pesa mingi. utafiti wa kutoka miaka sita hadi kumi inagharimu dola milioni mia mbili na thelathini na kwasababu hii utafiti unachukua muda mrefu kumalizwa lakini kuna utafifiti mbali mbali ambazo zinaendelea duniani.

Kuna vitu ambazo zianitwa Microbicides ambazo zinatumiwa kuteremsha nafasi ya kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi na zinafanana na mafuta au jeli. Microbicides bado hazijaanza kuuzwa lakini zinatarajiwa baada ya miaka tano. Microbicides pia zitatumika kujikinga kwa ugonjwa zote za zinaa na pia kuzuia mimba. Pia itaweza kutumika kwa muda mrefu, kile cha umuhimu ni kwamba hazitakuwa ghali na watu wote wa nchi zote wataweza kununua. pia zinaweza kutumika na kondomu. Utafiti unaendelea huko marekani ,uropa na Afrika na microbicides za kwanza zinatarajiwa kusaidia kwa asilimia arubaini hadi sitini(40% - 60%) na microbicides za pili zinatarajiwa kuwa asilimia sitini hadi themanini (60% - 80%) . Mwaka wa elfu mbii na saba utafiti huko afrika kusini zilifungwa kwasababu zilikuwa zian dhuru afya. Utafiti moja uliongeza nafasi ya wanawake kuambukizwa virusi lakini wana utafiti walisema wataendelea na njia zingine ambazo hazita dhuru afya.

Kuna madawa ambazo zinaitwa Pre-exposure prophylaxes na ambazo humezwa mara moja kwa siku na watu ambao hawana virusi ili kuwazuia kuapata virusi. Hizi madawa bado si kamili yaani asilimia mia moja na ni lazima zimezwe kila siku , utafiti wa madawa haya yanaendelea huko Botswana, Ghana, na Peru lakini matokeo yatatokea mwaka wa elfu mbili na nane au tisa.

Kutahirisha wanaume pia ni njia moja ya kumaliza ueneaji wa virusi. Utafiti uliofanyika mwaka wa elfu mbili na tano ulionyesha hatari ya kupatwa na virusi vya ukimwi uliteremshwa na asilimia sitini(60%) kwa wanaume ambao wametahiriwa , pia nchi ambazo wanaume wanatahiriwa ina watu kidogo ambao wana virusi vya ukimwi. Mahali pa kutahiri panapaswa kuwa pasafi na makali safi kutumika, pia kuna utafiti ambayo unaendelea kenya na uganda ili kuonyesha kama kutahiri kwa wanaume unapunguza nafasi ya wanawake kupata virusi hivi na matokeo yatatokea mwaka wa elfu mbili na saba.

Mwishowe njia nyingine ya kuteremsha kuenea kwa virusi vya ukimwi ni kuzuia ugonjwa unaoitwa herpes. Pande zingine za afrika asilimia sabini(70%) ya watu wako na ugonjwa huu wa herpes ,huko nchini Canada mtu moja kwa watu tano au sita ako na ugonjwa huu. Mwili hujaribu kutibu ugonjwa huu ambao huwa kidonda ,kama mtu akona na virusi basi virusi huingia kwa kidonda na ikasababisha ugonjwa wa ukimwi ni vizuri kuzuia ugonjwa huu wa herpes kwani husababisha mtu mwenye virusi kupata ugonjwa wa ukimwi. Utafiti unaendelea marekani kusini na Afrika na marekani kaskazini na matokeo yanatarajiwa mwaka elfu mbili na saba au nane.

Kwa miaka ishirini iliyopita pesa ya kuendeleza utafiti huu umetoka kwa serikali na jumuiya kadha. Ni vizuri kuelewa umuhimu ili kujua yakwamba kuna njia ambazo zinaweza kuzuia ugonjwa huu wa ukimwi. Tunafaiwa kufundisha jamaa na kufuata utafiti na kujifundisha njia za kujikinga kutokana na ugonjwa huu wa ukimwi.